

KUMB: PPR/16 - 10/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 5 Oktoba 2016**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 5 Oktoba 2016**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Septemba 2016. Kwa Mwezi Oktoba 2016, bei za rejareja kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimefungua kama ifuatavyo: TZS 12/lita sawa na asilimia 0.66, TZS 48/Lita sawa na asilimia 2.76 na TZS 15/Lita sawa na asilimia 0.91 sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa nazo zimefungua kama ifuatavyo: TZS 12.10/lita sawa na asilimia 0.70, TZS 48.29 sawa na asilimia 2.95 na TZS 15.19/lita sawa na asilimia 0.97. Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko haya yametokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia.
- (b) Bei za jumla na za rejareja kwa mafuta ya Petroli Dizeli na Mafuta ya Taa katika mkoa wa Tanga, nazo zimefungua ikilinganishwa na toleo la bei za mafuta hayo lililopita, la tarehe 07 Septemba 2016. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimefungua kwa viwango vifuatavyo: Petroli TZS 150/lita sawa na asilimia 7.74 Dizeli TZS 119/lita sawa na asilimia 6.53 na TZS 94/lita sawa na asilimia 5.34 sawia. Aidha, kwa kulinganisha matoleo haya mawili, bei za jumla zimefungua kama ifuatavyo: Petroli, TZS 149.53/lita sawa na asilimia 8.20, Dizeli, TZS 118.91/lita sawa na asilimia 6.94 na TZS 93.51/lita sawa na asilimia 5.69.
- (c) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana vile vile kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (e) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo ziwe chini ya bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 70/2016 la Mwezi Februari 2016.**

- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (g) Wanunuzi wahakikishewanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
Dar es Salaam	1,827	1,699	1,658
Arusha	1,911	1,783	1,742
Arumeru (Usa West)	1,911	1,783	1,742
Karatu	1,930	1,801	1,760
Monduli	1,917	1,788	1,748
Ngorongoro (Loliondo)	1,968	1,839	1,799
Kibaha	1,832	1,704	1,663
Bagamoyo	1,838	1,710	1,669
Kisarawe	1,835	1,706	1,665
Mkuranga	1,837	1,709	1,668
Rufiji	1,855	1,727	1,686
Dodoma	1,886	1,758	1,717
Bahi	1,893	1,765	1,724
Chemba	1,912	1,784	1,743
Kondoa	1,919	1,790	1,750
Kongwa	1,883	1,755	1,714
Mpwapwa	1,887	1,759	1,718
Iringa	1,891	1,763	1,722
Kilolo	1,896	1,767	1,727
Mufindi (Mafinga)	1,901	1,773	1,732
Njombe	1,919	1,791	1,750
Ludewa	1,957	1,829	1,788
Makete	1,950	1,822	1,781
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,917	1,789	1,748
Bukoba	2,042	1,914	1,873
Biharamulo	2,017	1,888	1,848

Karagwe (Kayanga)	2,059	1,930	1,890
Kyerwa (Ruberwa)	2,064	1,936	1,895
Muleba	2,042	1,914	1,873
Ngara	2,008	1,879	1,839
Misenyi	2,051	1,922	1,882
Geita	1,992	1,864	1,823
Bukombe	1,981	1,853	1,812
Chato	2,013	1,885	1,844
Mbogwe	2,030	1,902	1,861
Nyang'hwale	2,007	1,879	1,838
Kigoma	2,058	1,930	1,889
Uvinza (Lugufu)	2,070	1,942	1,901
Buhigwe	2,047	1,919	1,878
Kakonko	2,015	1,887	1,846
Kasulu	2,044	1,916	1,875
Kibondo	2,023	1,894	1,853
Moshi	1,901	1,773	1,732
Hai (Bomang'ombe)	1,904	1,776	1,735
Mwanga	1,894	1,766	1,725
Rombo (Mkuu)	1,922	1,794	1,753
Same	1,887	1,759	1,718
Siha (Sanya Juu)	1,907	1,779	1,738
Lindi	1,886	1,758	1,717
Kilwa Masoko	1,861	1,733	1,692
Liwale	1,907	1,779	1,738
Nachingwea	1,915	1,787	1,746
Ruangwa	1,913	1,785	1,744
Babati	1,950	1,821	1,780
Hanang (Katesh)	1,960	1,832	1,791
Kiteto (Kibaya)	1,961	1,832	1,791
Mbulu	1,962	1,834	1,793
Simanjiro (Orkasumet)	1,981	1,853	1,812
Musoma	2,006	1,877	1,836
Rorya (Ingirijuu)	2,014	1,886	1,845
Bunda	1,997	1,868	1,828
Butiama	2,002	1,874	1,833
Serengeti (Mugumu)	2,051	1,923	1,882
Tarime	2,017	1,888	1,847
Mbeya	1,934	1,806	1,765
Chunya	1,944	1,815	1,775
Ileje	1,947	1,819	1,778

Kyela	1,950	1,822	1,781
Mbarali (Rujewa)	1,918	1,790	1,749
Mbozi (Vwawa)	1,944	1,815	1,774
Momba (Chitete)	1,952	1,824	1,783
Rungwe (Tukuyu)	1,943	1,815	1,774
Morogoro	1,852	1,724	1,683
Mikumi	1,868	1,740	1,699
Kilombero (Ifakara)	1,890	1,762	1,721
Ulanga (Mahenge)	1,901	1,772	1,732
Kilosa	1,871	1,742	1,702
Gairo	1,871	1,742	1,702
Mvomero (Wami Sokoine)	1,863	1,734	1,694
Turian	1,877	1,749	1,708
Mtwara	1,900	1,771	1,731
Nanyumbu (Mangaka)	1,948	1,820	1,779
Masasi	1,925	1,797	1,756
Newala	1,932	1,803	1,762
Tandahimba	1,925	1,796	1,756
Mwanza	1,977	1,849	1,808
Kwimba	2,013	1,885	1,844
Magu	1,985	1,857	1,816
Misungwi	1,983	1,854	1,814
Sengerema	2,010	1,881	1,840
Ukerewe	2,037	1,908	1,867
Sumbawanga	2,000	1,872	1,831
Kalambo (Matai)	1,992	1,864	1,823
Nkasi (Namanye)	2,013	1,885	1,844
Katavi (Mpanda)	2,035	1,906	1,866
Mlele (Inyonga)	2,013	1,885	1,844
Songea	1,951	1,822	1,781
Mbinga	1,984	1,856	1,815
Namtumbo	1,980	1,851	1,811
Nyasa (Mbamba Bay)	1,986	1,858	1,817
Tunduru	2,009	1,881	1,840
Shinyanga	1,956	1,828	1,787
Kahama	1,970	1,841	1,800
Kishapu	1,984	1,856	1,815
Simiyu (Bariadi)	1,997	1,869	1,828
Busega (Nyashimo)	1,990	1,862	1,821
Itilima (Lagangabilili)	2,000	1,872	1,831
Maswa	1,989	1,860	1,820

Meatu (Mwanhuji)	1,996	1,867	1,827
Singida	1,918	1,789	1,749
Iramba	1,930	1,802	1,761
Manyoni	1,902	1,774	1,733
Ikungi	1,913	1,785	1,744
Mkalama (Nduguti)	1,942	1,814	1,773
Tabora	1,981	1,853	1,812
Igunga	1,935	1,807	1,766
Kaliua	1,999	1,871	1,830
Ulyankulu	1,993	1,865	1,824
Nzega	1,946	1,817	1,777
Sikonge	1,993	1,865	1,824
Urambo	1,994	1,866	1,825
Tanga	1,782	1,703	1,659
Handeni	1,803	1,724	1,680
Kilindi	1,818	1,739	1,695
Korogwe	1,794	1,715	1,671
Lushoto	1,804	1,725	1,681
Mkinga (Maramba)	1,789	1,710	1,666
Muheza	1,787	1,708	1,664
Pangani	1,789	1,710	1,666

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,719.41	1,591.00	1,550.24

Bei za Jumla-TANGA	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,674.10	1,595.24	1,551.08

Felix Ngamlagosi

**MKURUGENZI MKUU
EWURA**